# SHULE YA UPILI YA MARANDA

Cheti cha Kuhitimu Kisomo cha Sekondari

MTIHANI WA KITANGUIZI MWIGO 2023

**102/2 KISWAHILI (LUGHA) Karatasi ya 2**

**Aprili 2021 – Saa: 2½**

Jina : ........................................................... Nambari yaUsajili: ................

Mkondo: ............ Sahihi ya mtahiniwa: ................. Tarehe: ......../04/2023.

**Maagizo**

(a) *Andika jina lako na nambari yako ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*
(b) *Andika mkondo wa kidato chako kisha tia sahihi yako na uandike tarehe ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*
(c) *Jibu maswali* ***yote.***
(d) *Majibu yote* ***lazima*** *yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili.*
(e) *Majibu yote* ***sharti*** *yaandikwe katika nafasi ulizoachiwa katika kijitabu hiki cha maswali.*
(f) *Usitoe ukurasa wowote kutoka kwenye kijitabu hiki.*
(g) ***Karatasi hii ina kurasa 12 zilizopigwa chapa.***
(h) ***Watahiniwa lazima wahakikishe kwamba kurasa zote za karatasi hii zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.***

visit www.freekcsepastpapers.com to access more content

**Kwa Matumizi ya Mtahini Pekee**

| Swali | Upeo | Alama |
|---|---|---|
| 1 | 15 | |
| 2 | 15 | |
| 3 | 40 | |
| 4 | 10 | |
| Jumla | 80 | |

**1. UFAHAMU ( ALAMA 15)**

*Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.*

*(Mchana. Nyumbni kwa Mzee Njuga. Jua linawaka kwelikweli. Mkewe anawasili, mikononi ameshika pakiti moja ya unga wa dona.)*

*Mkoro:* Mume wangu, leo tungeshinda njaa. Kila muuzaji alikuwa hataki kuniuzia bila pesa taslimu. Hadi akatoka Mzee Faida na kunijalizia senti.

*Mzee Njuga:* Sasa unamwambia nani upuuzi huo?

*Mkoro:* Mume wangu, mazungumzo hayo yashakuudhi hivyo? Yashakuwa upuuzi?

*Mzee Njuga:* Kwa nini yasiniudhi? Sisi tubakije maskini ilhali tuna raslimali ya kujitajirisha?

*Mkoro:* (*Kwa mshangao*) Raslimali! Mbona hayajaniingia usemayo?

*Mzee Njuga:* Yatakuingiaje na jina lako halijakamilika? Wewe usingeitwa Mkoro, ungeitwa Mkorogo!

*Mkoro:* Yametoka wapi matusi?

*Mzee Njuga:* Kule yatokako kila siku! (*Mkoro anaingia ndani kujiepusha na ugomvi*) Kila siku tutakuwa watu wa kulipa karo tu na kukosa hata chakula? Alipiwaye karo ni msichana! Leo yuko darasa la saba na vibuzi vinamalizika. Je, akifaulu mtihani itakuwaje? Mimi sitangoja kiama hicho kiniangukie. Nitamwoza tu! Kwanza nitampeleka kwa Bi. Zee apitie ada ya usichana. Awe mwanamke kamili. (*Mkewe anatoka na kumsikiliza mumewe. Mzee Njuga hajui hayo)* Nitafanya vile nitakavyo! Hili ni boma langu!

*Mkoro:* Kefule! Unayoyazungumza ni mambo yaliyopitwa na wakati. Suala la kumwelimisha msichana limepewa kipaumbele katika karne hii. Mfumodume unaotazama mwanamke kama mtu wa kupika na kuchota maji umebadilika kitambo! Umepitwa na wakati.

*Mzee Njuga:* **Usinikerekete** masikio kwa hotuba yako isiyo na maudhui. Kaida ni binti yangu. Kwanza hayo mambo hayakuhusu.

*Mkoro:* Mimi ni mama yake. Lazima yanihusu. Uchungu wa mwana aujuaye mzazi!

*Mzee Njuga:* Na uchungu wa mzazi aujuaye nani? Hebu tuza makini. Ngoma isiyo yako usiivalie njuga.

*Mkoro:* Ngoma hiyo ya kumwoza Kaida nitaivalia nguja na kokwa.

*Mzee Njuga:* (*Kwa hasira*) Acha Kaida aje kutoka shule ndipo tujue yeye ni binti ya nani! *(Mara Kaida anatokeza. Amerudi nyumbani kwa chakula cha mchana)*

*Kaida:* (*Akimwamkua mamake*) Shikamoo mama!

*Mkoro:* Marahaba binti yangu. Umeshindaje?

*Kaida:* Vema mama. (*Akimwamkua babake*) Shikamoo baba!

*Mzee Njuga:* Marahaba! (*Akimgeukia mkewe*) Hebu tuzungumze sasa, Kaida amekuja. (*Akiita*) Kaida njoo hapa.

visit www.freekcsepastpapers.com to access more content

*Mkoro:* Mwache mtoto ale kwanza. Hata hajapumzika! Huoni kuwa jua liko utosini na wewe ndio mwanzo unataka kumsumbua.

*Kaida:* (*Anashangaa kwa mazungumzo hayo yasiyokuwa ya kawaida*) Kuna nini mama? Nimewakosea au nini baba?

*Mzee Njuga:* Hujakosea. Ni mazungumzo tu ya maisha.

*Kaida:* Basi naomba mnieleze wazazi wangu nisingependa nichelewe kurudi shuleni mchana.

*Mzee Njuga:* (*Huku akijitayarisha kuondoka*) Nitakueleza jioni.

*Mkoro:* Chakula? Kwani hutaki kula?

*Mzee Njuga:* Nitakula nirudipo.

*(Mama akila na binti yake)*

*Mkoro:* Kaida, mimi ni mamako na nakupenda sana. Babako pia anakupenda.

*Kaida:* Najua mama. Nyote mnanipenda ndio maana mnanisomesha. Nyinyi si kama wazee wengine hapa kijijini waliowaoza mabinti zao kwa tamaa ya pesa. Na mimi nawaahidi matokeo mazuri mwaka ujao. Si unajua hakuna mwanafunzi anayenishinda tangu darasa la kwanza?

*Mkoro:* Najua yote hayo. Ninakuombea Maulana nyota yako izidi kung'ara masomoni.

*Kaida:* Amina mama!

*Mkoro:* Jambo ambalo sitakuficha ni kuwa babako amekuwa mumunye kuharibikia ukubwani!

*Kaida:* Unamaanisha nini mama?

*Mkoro:* Babako ana wimbo anaimba. Wimbo huo ni mui na wimbo mui haungolewi mwana. Mimi ni lazima nikueleze asemayo baba yako kwani mficha maradhi hufichuliwa na kilio.

*Kaida:* (*Kwa kushtuka, anaacha kula*) Baba ana nini? (*Anaanza kulia*) Niambie baba amepatwa na baa gani?

*Mkoro:* (*Akimtuliza*) Tulia Kaida nikueleze. Si jambo la kukuliza kwani lingeniliza mimi kwanza na ungekuja na kupata mto wa machozi hapa ukitiririka hadi baharini. Ni jambo linalohitaji ujasiri mkubwa.

*Kaida:* (*Bado anaonyesha wasiwasi*) Kwa nini usiniambie?

*Mkoro:* Babako anataka eti akuachishe shule ili akuoze!

*Kaida:* Hilo haliwezekani! Mimi nataka nisome niwe rubani. Mambo ya kuolewa yako mbali na fikra zangu. Ama ni mpango wenu nyinyi nyote?

*Mkoro:* Mimi simo! Ni huyo babako.

*(Mara sauti ya mifugo inasikika. Mbuzi, ng'ombe na kondoo wanajazana shambani mwa Mzee Njuga kula mahindi. Mama anachukua mpweke kuwatoa)*

*Mchungaji:* (*Ameacha kupiga mbinja ya kuwaongoza mifugo. Anaongea kwa sauti ya juu*) Mama Kaida, usiwapige. Hawa sasa wamefika kwao.

*Mkoro:* (*Kwa mshangao*) Eti wamefika kwao!

visit www.freekcsepastpapers.com to access more content

*Mchungaji:* Kwani mlitaka mahari ya nini? Si mlitaka ng'ombe kumi, mbuzi ishirini na kondoo saba? Acha ng'ombe wale mahindi yao. Tena unipe shilingi hamsini za kuwaletea mifugo wenu. Huyo Mzee Njuga nikimsubiri atanichelewesha.

*Mkoro:* Tafadhali kijana. Usiniweke roho juujuu na huo upuuzi wenu. Kwanza nenda ukadai pesa kwa aliyekutuma. Mzumbua chungu ndiye mpishi. Tena ninamngoja aniambie hayo mambo ya mahari.

*(Mzee Njuga anafika. Anaandamana na Bi. Zee na mzee mwingine aliyekonga mno)*

*Bi. Zee:* (*Akiimba wimbo wa tohara*)
Haya! Twaja kurembesha mwari.
Haya! Twaja kupamba jukwaa.
Yu wapi eee!
Yu wapi eee!
Binti mchanga tumkuze akomae
Yu wapi eee!
Avushwe daraja aingie utu uzima!

*(Kaida anashtuka. Anaona hatari inayomkabili. Anatimua mbio hadi shuleni na kumweleza mwalimu mkuu. Mwalimu naye anapiga simu kwa polisi. Kabla ya polisi kufika kwa Mzee Njuga , mzee aliyepangiwa kumwoa Kaida amekasirika)*

*Mzee Kale:* Mimi sikuja kutazama hiki kibanda chako, nimeletwa na posa. Niozeshe binti haraka niende na mke wangu.

*Mzee Njuga:* (*Kwa mkewe* ) Mbona umemtorosha binti yangu? Unataka kunitia aibu siyo?

*Mkoro:* Kaida hawezi kuolewa na kuacha masomo yake!

*Mzee Kale:* *(Akitetemeka kwa hasira)* Mimi sibanduki hapa hata ufanye mazingaombwe gani. Nimtakaye ni Kaida. Unauwasha moto, kuuzima wacheza sengenya? Umechukua mifugo wangu na unitembeze maili zote hadi hapa. Naona asali itageuka shubiri.

*Mzee Njuga:* (*Akimsihi* ) Ngoja bwa mkubwa. Niache nipige mbiu na nitafute vijana waliokula wakashiba wakamtafute.

*(Mara Kaida anafika akiongozana na askari tisa, mwalimu mkuu, mama wa maendeleo kijijini, afisa wa watoto na wakili wa kutetea haki za kina mama na watoto . Gari la mkuu wa wilaya linafika pia)*

*Kaida:* Hapa ndipo nyumbani na hawa ndio wazazi wangu. (*Mzee Kale na Bi. Zee wanajaribu kukimbia. Wanakamatwa. Wote wanatiwa garini. Mzee Njuga anatiwa pingu)*

*Mzee Njuga:* Nimefanya nini? Kaida ni binti yangu.

*Polisi:* Hayo utayaeleza mahakamani.

*(Baada ya majuma mawili gazeti la* ***Haki Zenu*** *linachapisha kichwa cha habari: MZEE AFUNGWA MIAKA MITANO KWA KUTAKA KUMWOZA BINTIYE WA DARASA LA SABA)*

visit www.freekcsepastpapers.com to access more content

a) “Suala la maendeleo ya msichana limepewa kipaumbele katika karne hii.” Thibitisha kwa mujibu wa kifungu. (alama 4)

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

b) Mzee Njuga anazingatia mambo ambayo yamepitwa na wakati. Eleza. (alama 3)

visit www.freekcsepastpapers.com to access more content

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

c) Tofautisha Mzee Njuga na Mkoro kama wazazi. (alama 2)

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

d) Fafanua ‘wimbo’ ambao Mzee Njuga aliuimba kila wakati. (alama 1)

..........................................................................................................................................

e) “Naona asali itageuka kuwa shubiri.” Eleza hali hii inavyodhihirika kifunguni. (alama 2)

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

f) “Tamaa mbele mauti nyuma.” Eleza sifa hii inavyomwafiki Mzee Njuga. (alama 2)

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

g) Andika kisawe cha neno “**Usinikerekete”** kama lilivyotumika kifunguni. (alama 1)

..........................................................................................................................................

**2. UFUPISHO ( ALAMA 15)**

*Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali*

Maadili ni desturi, utamaduni au hulka ambazo hubainisha na kulipa kundi fulani la watu upekee wake. Maadili ni muhimu katika kuonyesha imani na kanuni za maisha ambazo kundi fulani la watu huchukulia kuwa chanya na zile wanazozichukulia kuwa hasi. Maadili ndio mwongozo unaothibiti matendo na hulka za kila mmoja. Kila jamii huwa na maadili yake ambayo yanamhitaji kila mwanajamii kutenda na kuishi kama jamii inavyotarajia. Maadili hutusaidia kubainisha sisi ni akina nani, mtazamo wetu maishani, pamoja na matarajio yetu.

Katika katiba ya Kenya, maadili ya jamii ya Wakenya yameangaziwa vyema. Kwanza, ni wazi kuwa Kenya ni taifa la wacha mungu, kwa hivyo, kila Mkenya anatarajiwa kuabudu na kumheshimu Mwenyezi Mungu. Hili limeshadidiwa hata katika wimbo wetu wa taifa. Pamoja na hayo, katika kuimarisha umoja wa kitaifa, tofauti zetu Wakenya kirangi, kikabila, kitabaka na hata kidini hazipaswi kutugawanya. Maadili yanatuhimiza kuzichukulia hizo kuwa sifa za kipekee na kuzionea fahari. Ule utaifa wetu kama Wakenya unapaswa kuwekwa mbele daima ili kuzima juhudi zozote za kututenganisha kwa misingi hiyo.

Kama taifa, tunahitaji kudumisha uzalendo wetu kwa kujitolea kuhakikisha kuwa mahasidi hawaporomoshi maadili ya jamii zetu kwa kuiga hulka zao potovu. Uzalendo unatuhumiza kuripoti vitendo vyote vya kuihujumu nchi au watu wake kwa asasi za dola. Asasi hizo zitachunguza na kuzima utekelezaji wa uhalifu kabla haujatokea, na iwapo utakuwa umetokea, asasi hizo zitawapa adhabu wahalifu ili waweze kubadili mienendo mibaya na kuwa kielelezo kwa wengine wenye nia mbaya.

Maadili, vilevile, humwongoza mtu kuhusu namna za kutatua mizozo na kudumisha amani. Hatuwezi tukajivunia uhuru pasi na kuwepo amani. Amani ndio msingi wa umoja, ustawi na maendeleo ya taifa lolote. Ukosefu wa amani hudumaza na hata kurudisha nyuma maendeleo kwa kuwahini watu nafasi za kushiriki uzalishaji mali. Ukosefu wa amani vilevile husababisha kuongezeka kwa visa vya uhalifu kama vile mauaji, kulemazwa kwa watu, unajisi, uharibifu wa mali na kusambaratika kwa familia, hali ambayo huchangia mporomoko wa maadili katika jamii.

Utiifu wa sheria vilevile ni njia mojawapo ya kukuza maadili ya kijamii. Kwa kuwa sheria hulinda haki za kila mtu; wake kwa waume, wakubwa kwa wadogo, kila mmoja ana wajibu wa kuheshimu sheria. Hii ni pamoja na kulinda rasilimali zetu kama jambo la wajibu bila ya kutegemea kuwepo wadumisha sheria. Uongozi wa kisheria huwapa watu hakikisho kuwa maisha yao hayatakuwa kama ya mahayawani nyikani bali yatafuata utaratibu fulani. Hivyo basi, sheria ni hakikisho la jamii inayolinda haki na kuendesha mambo yake kwa uwazi, haki na ushwari.

Uadilifu unakwenda kinyume na methali, amani haiji ila kwa ncha ya upanga. Ukweli ni kwamba, tunaweza kusuluhisha tofauti zetu bila kutumia silaha. Matumizi ya silaha aghalabu huzidisha uhasama na kuchochea haja ya kulipiza kisasi. Njia pekee ya kutatua migogoro ni kuelewa chanzo cha migogoro yenyewe, wahusika kufanya kikao na kuizungumzia kwa uwazi na kwa utulivu. Pande zote husika zinafaa kukubali makosa au madhara yaliyotokana na

visit www.freekcsepastpapers.com to access more content

matendo yao na kuomba msamaha ili kupata maridhiano. Kuomba msamaha kusidhaniwe kuwa kujishusha hadhi, bali ni unyenyekevu katika kutatua tofauti kwa manufaa ya muamala wa vizazi vijavyo. Anayeombwa msamaha naye anapaswa kuwa tayari kutoa shifaa kwa dhati na kusahau kosa alilofanyiwa. Yote haya yakishindikana, mgogoro wapaswa kupelekwa mahakamani. Haki za kila mmoja zimelindwa katika katiba yetu na mahakama zipo ili kutetea haki hizi bila kupendelea upande wowote.

Bila shaka, tukizingatia na kuimarisha maadili, taifa letu litakuwa jamii bora na kivutio cha kila mtu. Kiu ya Wakenya ya kutaka kuhamia nchi nyingine, hasa zilizostawi, itapungua. Wote watakuwa na ari ya kuliendeleza taifa lao.

a) Dondoa mambo muhimu yanayojitokeza katika aya za kwanza tano. (maneno 90 – 100)
   ( alama 10 , 1 ya utiririko)

**Matayarisho**

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

visit www.freekcsepastpapers.com to access more content

**Jibu**

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

.......................................................................................................................................

.......................................................................................................................................

.......................................................................................................................................

.......................................................................................................................................

.......................................................................................................................................

.....................................................................................................................................

.......................................................................................................................................

.......................................................................................................................................

.......................................................................................................................................

b) Ukirejelea aya za mwisho mbili, fafanua jinsi mizozo inaweza kutatuliwa kwa uadilifu. (maneno 40 – 45) (alama 5, 1 ya utiririko)

**Matayarisho**

.......................................................................................................................................

.......................................................................................................................................

.......................................................................................................................................

.......................................................................................................................................

.......................................................................................................................................

**Jibu**

visit www.freekcsepastpapers.com to access more content

.......................................................................................................................................

.......................................................................................................................................

.......................................................................................................................................

.......................................................................................................................................

.......................................................................................................................................

.......................................................................................................................................

**3. MATUMIZI YA LUGHA (ALAMA 40)**

a) Andika maneno yanayoafiki maelezo haya: (alama 2)

i. Irabu ya nyuma juu, kipasuo sighuna cha midomoni, kiyeyusho cha kaakaa gumu, irabu ya chini.

.............................................................................................................................................

ii. Kipua ghuna cha kaakaa laini, irabu wastani mviringo, sauti mwambatano ya midomo, irabu ya mbele kati

…………………………………………………………………………………………………

b) Andika neno lenye muundo ufuatao ya silabi: IKIKI (alama 1)

.............................................................................................................................................

c) Eleza majukumu ya kisarufi ya mofimu katika neno "**lililochika**." (alama 3)

.............................................................................................................................................

.............................................................................................................................................

.............................................................................................................................................

d) Andika sentensi ifuatayo upya ukitumia neno lililopigwa mstari kama nomino. (alama 2)

Tembo <u>alicheka</u> hadi akawaudhi wengi.

.............................................................................................................................................

e) Andika sentensi ifuatayo kwa wingi:- (alama 1)

Ua uliokauka utakatwa na bawabu

.............................................................................................................................................

f) Tunga sentensi ukitumia kiwakilishi kisisitizi cha wastani katika ngeli ya U – I umoja (alama 2)

.............................................................................................................................................

g) Unganisha sentensi zifuatazo ili uwe na sentensi yenye kishazi tegemezi. (alama 2)

Tumaini atacheza vizuri.

Tumaini atazawidiwa pesa.

.............................................................................................................................................

visit www.freekcsepastpapers.com to access more content

h) Akifisha sentensi ifuatayo: (alama 2)

enhe tena lilia baba akauliza

..........................................................................................................................................

i) Andika sentensi ifuatayo katika hali ya udogo. (alama 2)

Ndege mkubwa ana miguu miembamba.

..........................................................................................................................................

j) Geuza sentensi ifuatayo kwa wakati ujao hali timilifu. (alama 2)

Kikwai alipakia shehena katika jahazi.

..........................................................................................................................................

k) Changanua sentensi ifuatayo kwa kielelezo cha matawi. (alama 3)

Zilikuwa zashughulikia zote vizuri

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

visit www.freekcsepastpapers.com to access more content

l) Tambua matumizi ya kiambshi **u** katika sentensi ifuatayo. (alama 3)

Unaona vile usomi wake ulivyomfaidi maishani.

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

m) Andika sentensi ifuatayo upya ukibadilisha yambwa tendewa kuwa kiima. (alama 2)

Salihina atawaletea wanafunzi zawadi.

..........................................................................................................................................

n) Tambua kijalizo katika sentensi ifuatayo. (alama 1)

Watu hao wanne walikuwa watumwa wote.

..............................................................................................................................................

o) Tunga sentensi yenye muundo ufuatao. (alama 2)

KN(V + N) + KT (T + N + RH)

..............................................................................................................................................

..............................................................................................................................................

p) Vitabu vilipopotea muktubi alikuwa na wasiwasi. (alama 2)

Anza kwa: Kupotea ...

..............................................................................................................................................

q) Andika maana **mbili** zinazodhihirika katika sentensi ifuatayo. (alama 2)

Luka alimwona Asna akiwa darasani.

..............................................................................................................................................

..............................................................................................................................................

..............................................................................................................................................

r) Kanusha sentensi ifuatayo. (alama 2)

Sabina hupita hapa, huenda ukampata.

..............................................................................................................................................

s) Tunga sentensi **moja** kutofautisha kimaana maneno **fuka** na **vuka**. (alama 2)

..............................................................................................................................................

..............................................................................................................................................

t) Tunga sentensi ukitumia kihusishi cha daraja. (alama 1)

..............................................................................................................................................

u) Tunasema tita la kuni na ........................... ya mlima, nao hawa wawili wana urafiki wa ........................................................................ (alama 1)

visit www.freekcsepastpapers.com to access more content

**4. ISIMUJAMII (ALAMA 10)**

"Mwenye sikio amesikia. Usiwe kama mimi. Waambae wote wakupotoshao. Fuata kielelezo cha wanaokujali. Kwangu nimejishika sikio baada ya laiti nyingi. Macho yamefumbuka sasa. Lengo langu ni kuwahi uzamili na hata uzamifu. Kwani kuitwa profesa ni kosa? Tunachohitaji, ni ujasiri wa simba kuyakabili masomo. Adabu na bidii yetu leo, ni miche itakayozaa matunda matamu ya maisha mema kesho. Tukumbuke kesho hujengwa leo."

a) Tambulisha sajili ya mazungumzo haya kwa kuzingatia vigezo vifuatavyo: (alama 2)

i. Dhamira / maudhui

....................................................................................................................................................

ii. Mazingira / mahali

....................................................................................................................................................

b) Eleza sifa za lugha zilizotumika kwenye mazungumzo haya. (alama 5)

....................................................................................................................................................

....................................................................................................................................................

....................................................................................................................................................

....................................................................................................................................................

....................................................................................................................................................

....................................................................................................................................................

....................................................................................................................................................

....................................................................................................................................................

visit www.freekcsepastpapers.com to access more content

c) Eleza jinsi madhumuni yanavyoathiri mitindo ya lugha. (alama 3)

....................................................................................................................................................

....................................................................................................................................................

....................................................................................................................................................

....................................................................................................................................................

....................................................................................................................................................

Matumizi ya lugha.

(

(b) Ajapo
alapo
ajaye n.k

*(1 x 1 = al 1)*

(c) Aliyekisahau
Tanbihi - mzizi uwe wa kitenzi cha asili ya kigeni. *2/0*

(d) Kucheka kwa Maria kuliwashangaza wengi au
Kicheko cha Maria kiliwashangaza wengi. *2/0*

(e) Nyua zilizokauka ni za mabawabu. *1/0*

(f) Mifano ya nomino katika ngeli ya l - l
Kama vile sukari, petroli, chumvi.
Sukari iyo hiyo ilimwagika. n.k *2/0*

(g) Kidege hiki kina viguu vidogo. *1/0*

(h) Kembo akiimba vizuri atatuzwa zawadi.
Kembo aimbapo vizuri atatuzwa zawadi.
Iwapo Kembo ataimba vizuri atatuzwa zawadi.
Ikiwa Kembo ataimba vizuri atatuzwa zawadi. *2/0*

(i) (i) Kubainisha maneno ya lugha nyingine yanayoingizwa katika lugha ya Kiswahili.
(ii) Kufungia majina ama anwani za vitabu, nyimbo, filamu. n.k *2/0*
(iii) Kufungia maneno yasiyozoeleka au ambayo hayajakubalika kama msamiati wa lugha fulani .
Mambo yakiwa "poa".
(iv) Kufungia neno lenye maana tofauti na iliyokusudiwa yeye ni "karimu" ukimaanisha ni bahili.

*(2 x 1 = a 2)*

(j) Kuli hatakuwa amepakia shehena katika meli. *2/0*

(k)

(m) Wanafunzi watasimuliwa hadithi na mwalimu. *2/0*

(n) watumwa

*(1 x 1 = al 1)*

(o) mfano:
Yeye atawaimbia wageni wa rais. *3/0*

(p) nikahi / nikaha
mimba / ujauzito

*(2 x 1 = al 2)*

(q) kirimu / mzee aliwakirimu wanakijiji. *2/0*

(r) (i) Ishallah! kutakia heri.
(ii) Simile - Kutoa ombi la kupishwa.

*(2 x 1 = al 2)*

(s) Fuka - toa moshi
- sababisha kunukia
Vuka - toka upande mmoja hadi mwingine.
- zidi kiasi
- potoka

visit www.freekcsepastpapers.com to access more content

- kuwa uchi / toka nguo *2/0*

(t) Mchelea mwana kulia hulia yeye
Mtoto umleavyo ndivyo akuavyo. *1/0*

(u) Kupotea kwa mbuzi kulimtia mchungaji wasiwasi. *2/0*

*(Adhibu makosa sita ya hijai 6 x $^1/_2$ = al 3, ondoa nusu alama kwa kila kosa la sarufi, usiadhibu zaidi ya nusu ya alama uliyotuza)*

**a) Taja sajili ya mazungumzo haya. (alama 2)**

I. Sajili ya mawaidha/ushauri/ wosia/ nasaha - Mzungumzaji anamtolea msikilizaji nasaha asifuate mkondo mbaya wa maisha aliyofuata.
II. Shuleni/chuoni/taasisi ya elimu – anaiotoa nasaha hii kwa wenzake akiwa chuoni kwa sababu anasema lengo ni kupata shahada.

**b) Eleza za lugha iliyotumika kwenye mazungumzo haya. (alama 5)**

- Lugha iliyojaa matumini-anawania kupata uzamili na uzamifu
- Utohozi-profesa-professor
- Swali balagha-kwani kuitwa professor ni kosa.
- Iv) Lugha ya kuonya-mwenye sikio amesikia
- Nahau-nimejishika sikio-nimejirekebisha
- Lugha sanifu-Kifungu kizima kimetumia lugha ipasavyo
- Lugha ya maelezo- Waambae wote wakupotoshao. Fuata kielelezo cha wanaokujali.
- Msemo-macho yamefumbika-amezinduka
- Matumizi ya msamiati wa taaluma ya kiusomi-uzamili,uzamifu na profesa
- Matumizi ya sentensi fupi fupi-Usiwe kama mimi.
- Lugha inayotumia taswira-anapotolea nasaha anasema usiwe kama mimi picha ya pengine jinsi alivyoathirika anajitokeza akilini.
- Lugha imejaa hekima-anasema fuata kielelezo ha wanaokujali(Ushauri anatoa unaongozwa na busara kwa yule hataki msikilizaji ahasirike)

c) **<u>Madhumuni</u>**

- Lengo la mawasiliano huathiri toni anayoitumia mtu, kwa mfano, akitaka kushawishi, atatumia toni ya upole, akitaka kukemea atatumia toni kali
- Lengo huathiri uteuzi wa msimbo, kwa mfano mtu akitaka kujihusisha na watu wa jamii fulani atatumia lugha yao. Hii ndiyo sababu ya baadhi ya wanasiasa kutumia sheng' wanapozungumza na vijana ili kujihusisha nao.
- Madhumuni huathiri kiimbo. Mtu anaweza kupandisha sauti yake akitaka kusisitiza jambo.
- Madhumuni huathiri shadda katika lugha. Mtu huweka shadda katika maneno yale anayotaka kusisitiza.
- Madhumuni huweza kuathiri uteuzi wa msamiati. Mtu akitaka kujionyesha kuwa msomi, atateua maneno katika lugha yake yatakayomfanya kuafikia lengo lake.
- Madhumuni huathiri usanifu wa lugha. Mtu akitaka kuburudisha na kuchekesha, atasongoa lugha kimakusudi ili watu wacheke.
- Madhumuni huathiri tafdsida katika lugha. Mtu akitaka kukasirisha, anaweza kutumia lugha kali isiyokuwa na tasfida ndani yake.

visit www.freekcsepastpapers.com to access more content